TANGAZO LA SERIKALI NA. 1035 la tarehe 13/12/2024

SHERIA YA MISITU,

(SURA YA 323)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 23(1))*

NOTISI YA KUSUDIO LA KUTANGAZA ENEO LA MSITU WA MTO MZOMBE KUWA MSITU WA HIFADHI YA TAIFA MTO MZOMBE YA MWAKA 2024

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kutangaza Eneo la Msitu wa Mto Mzombe kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Mto Mzombe ya Mwaka 2024.

Eneo linalopendekezwa kutangazwa

2. Eneo la msitu lililo ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Mto Mzombe.

Madhumuni ya tangazo

3. Madhumuni ya kupendekezwa kutangaza Msitu wa Hifadhi wa Taifa Mto Mzombe ni-

(a) kulinda eneo lililo hatarini la misitu, nyasi, miti ya miombo na ardhi oevu ambalo linatambulika kwa thamani yake ya juu ya baioanuwai, lenye upekee wa mimea na wanyama, ikijumuisha aina za mimea na wanyama walio hatarini kutoweka; na

(b) kulinda eneo la msitu na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu katika eneo la msitu huo.

Uhalali wa Notisi

4.-(1) Notisi hii itakuwa halali kwa muda wa siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

(2) Ndani ya kipindi hicho cha siku tisini, mtu au kundi la watu au mwakilishi wao anaweza, kwa maandishi kuwasilisha pingamizi, maoni au madai ya haki yoyote inayotokana na sheria za kimila kuhusiana na ardhi au mazao ya msitu au haki yoyote iliyoainishwa kwenye

sheria nyingine katika eneo ambalo linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Mto Mzombe.

Uwasilishaji wa pingamizi

5. Pingamizi, maoni au madai yoyote dhidi ya kusudio la kutangaza eneo la Msitu Mto Mzombe kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Mto Mzombe, yawasilishwe ndani ya siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii kwa anuani ifuatayo:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maliasili na Utalii,
S.L.P. 1351,
DODOMA.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*


WILAYA YA CHUNYA

MSITU WA HIFADHI WA TAIFA MTO MZOMBE

Makadirio ya eneo: Hekta 73,116 au Kilometa za Mraba 731.16

Unakopatikana na Mipaka:
Eneo lote la hifadhi awali chini ya Eneo la Msitu wa Mto Mzombe unaopatikana Wilaya ya Chunya katika Mkoa wa Mbeya kama lilivyochorwa katika Ramani Na. Jb 3177 (Skeli 1:50,000) iliyohifadhiwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani na lenye mipaka ifuatayo:

*Tangazo la Serikali Na. 1035 (Linaendelea)*




Dodoma,
11 Novemba, 2024

PINDI HAZARA CHANA
*Waziri wa Maliasili na Utalii*